HALMASHAURI YA MJI KASULU

(*Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji****)***

Simu/Fax 255-028-2810355
S.L.P. 475.

Mhe: Mwenyekiti

Mkutano wa Baraza la Madiwani

MJI- KASALU.

YAH: TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI KATIKA KIPINDI CHA (JANUARI-MACHI 2017) KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017).

Mhe Mwenyekiti ifuatayo ni taarifa ya kamati ya kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha Januari-Machi 2017. Aidha kamati hii inaundwa na idara zifuatazo:-

- Idara ya Fedha na Biashara
- Idara ya Utumishi na Utawala
- Idara ya Mipango na Ufuatiliaji
- Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
- Kitengo cha Manunuzi na Ugavi
- Kitengo cha Sheria
- Kitengo cha TEHAMA

Mhe. Mwenyekiti mhutasari wa taarifa ya kazi kwa kila idara umeambatanishwa katika taarifa hii.

Naomba kuwasilisha.

Mh.Deusi Kibabi

Makamu Mwenyekiti

Halmashauri ya Mji- KASULU

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI JANUARI -MACHI 2017

- Mhe.Mwenyekiti,Halmashauri ya Mji-Kasulu kwa Mwaka wa fedha 2016/2017 ilikisia kupata jumla ya Tshs. 31,620,149,988 ikiwa ni mapato yote ya Halmashauri kwa mchanganuo ufuatao:-

S/N	KIFUNGU CHA MAPATO	KIASI
1	Mapato ya ndani kutoka vyanzo mbalimbali	1,035,082,000
2	Mapato ya ndani yenye masharti (Bima ya Afya,Ada ya kila siku na CHF)	587,200,000
3	Fedha za Fidia ya vyanzo vilivyofutwa	158,866,000
4	Fedha ya Ruzuku ya matumizi ya kawaida(OC)	1,352,782,000
5	Fedha za Miradi ya Maendeleo	7,956,706,200
6	Fedha za Mishahara	20,529,513,788
	JUMLA YA MAPATO YOTE	**31,620,149,988**

Mhe:Mwenyekiti kwa kipindi mpaka kufikia mwezi machi 2017 Halmashauri ya Mji wa Kasulu ilikusanya Tshs.87,119,918,.57 (TZS 73,691,918.57) mapato ya ndani yasiyo na mashariti, na TZS 13,428,000/= mapato ya ndani yenye mashariti-Bima, CHF, USER FEES) kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani (Own sources).

Jumla ya makusanyo yote ya mapato ya ndani yasiyo na mashariti Julai 2017 hadi Machi, 2017 ni TZS 565,457,429.51 sawa na asilimia 55.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Kasulu kwa mwezi Machi, 2017 imepokea fedha kutoka serikali kuu – Mfuko wa Barabara kiasi cha Tzs 141,109,688.31/= **,** UNICEF kiasi cha TZS 15,539,000 ,TASAF Kiasi cha TZS 171,841,500,Madeni ya walimu kiasi cha TZS 18,579,000/= kwa mchanganuo ufuatao.

S/NA	**AINA YA MAPATO**	**KIASI**
1	Mfuko wa Barabara	141,109,688.31
2	TASAF	171,841,500.00
3	Fedha za UNICEF	15,539,000.00

4	Madeni ya walimu	18,579,000.00
JUMLA KUU		**347,069,188.31**

2 : MATUMIZI

Mhe.Mwenyekiti hadi kufikia mwezi marchi Halmashauri imeweza kutumia kiasi cha **Tshs 357,840,968.92/=**kwa machanganuo ufuatao:-

S/N	**AINA YA CHANZO CHA MATUMIZI**	**KIASI**
1	**MapatoyaNdani**	70,008,885.95/=
2	MfukowaBarabara (Road Fund)	1,450,000/=
3	OC Elimusekondari	3,000,000/=
4	Fedhazakunusuru kaya Masikini(TASAF)	167,718,896.46/=
5	MfukowaPamojawaAfya (Busket Fund)	8,420,000/=
8.	CBG utawala	13,310,000/=
8	Ada yaTiba	11,000,000/=
9	Equip elimu	6,805,000/=
10	CDG mipango	8,590,000/=
11	Kigoma grand high school	46,362,305/=
12	Mfuko wa jimbo	561,381.5/=
13	OC Elimu msingi	20,212,000/=
JUMLA YA MATUMIZI		**357,840,968.92/=**

- Katika kipindi cha robo ya tatu yaani Januari hadi Machi 2017, Kamati ilipitia taarifa ya ukaguzi wa Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani za Halmashauri. Katika kipindi hicho Kitengo cha Halmashauri kupitia Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, imeendelea kutekeleza ukaguzi katika Idara na Vitengo vyote vya Halmashauri katika Akaunti zote za Halmashauri,kama Akaunti ya Matumizi Mengineyo (Other Charges (OC),Akaunti ya barabara (Road Fund A/C), Akaunti ya Amana (Mesceleniuos A/c), Akaunti ya Maendeleo (Development

A/C), Akaunti ya mapato ya Ndani (Own source A/C), Miradi inayotekelezwa na Halmashauri kwa mwaka wa Fedha ya mwaka 2016/2017. Hata hivyo Kitengo cha Ukaguzi kimeendelea kufuatilia utekelezaji wa majibu ya menejimenti kwa hoja kumi na tatu(13) mpya na kujibiwa hoja zote,pamoja na Hoja moja (1) ya mwaka wa fedha 2015/2016 na hoja nne (4) ya robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2016/2017 zilizoibuliwa wakati wa ukaguzi.

- Aidha Halmashauri kupitia Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani za Halmashauri, kwa kushirikiana na Idara ya Ujenzi kimeweza kukamilisha ukaguzi wa Mradi wa utengenezaji wa barabara za Kasulu Mjini wenye thamani ya TZS 126,473,000/= kwa Mkataba Na : LGA/168/2015/16/W/02 ,Mkandarasi M/S WESTBLACKS GENERAL ENTERPRISES ambapo Mkataba huu ulivunjwa baada ya kukiuka masharti kwa mujibu wa kifungu cha sheria ya Mikataba Clause 62 section.2 sub – section (a),na baadaye kazi hiyo ikafanywa na Mkataba na LGA/2016/2017/HQ/W/02/01 ,Mkandarasi MALAGARASI ENTERPRISES CO. wenye thamani ya TZS 81,586,000/=. Na ujenzi huo unaendelea.
- Pia Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwa kushirikiana na Idara Ya Maji ya Mji,kimeweza kukamilisha ukaguzi katika utengenezaji wa Miradi Mitatu ya Maji inayofadhiliwa na Wizara ya Maji (WSDP) , Miradi hiyo ni (1) Mradi wa Maji wa Heru Juu wenye thamani ya TZS477,465,500/= kwa mkataba Na. LGA/168/2016/2017/W/01/02 ,Mkandarasi M/S VUMWE GENERAL SERVICES AND SUPPLIES CO.LTD, (2) Mradi wa Maji Kimobwa wenye thamani ya TZS 428,400,000/= kwa Mkataba LGA/168/2016/2017/W/01/02 ,Mkandarasi VUMWE GENERAL SERVICES AND SUPPLIES CO.LTD, (3) Mradi wa Maji Muhunga wenye thamani ya TZS 329,587,000/= kwa Mkataba Na. LGA/168/2016/2017/W/01/01 ,Mkandarasi M/S DYNOTECHENGINEERING LTD,. Na ujenzi huo unaendelea. Pia kwa robo hii ya tatu kwa mwaka wa Fedha 2016/2017, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani wa Halmashauri kiliendelea kutoa ushauri kwa menejimeti juu ya kuzingatia matumizi sahihi ya Bajeti ya mwaka

2016/2017 kwa kuzingatia vifungu sahihi vilivyoainishwa kwenye Bajeti katika kila Idara na Vitengo,sambamba na matumizi ya Votebook.

- Katika kipindi cha robo ya tatu yaani Januari hadi Machi 2017, Kamati ilipitia taarifa ya Kitengo cha TEHAMA kimeweza kusimamia uhamishaji wa mfumo wa mapato kutoka server ya Halmashauri ya Mji Kasulu (local server) na kuupeleka kwenye server kubwa TAMISEMI(Main server), ufungaji wa mfumo wa Fedha (EPICOR 10) kwa kushirikiana na wataalamu toka TAMISEMI ,kutengeneza mtandao kiambo (LAN) katika Hospitali ya Wilaya Kasulu kwa ajili ya maandalizi ya kufunga mfumo wa kukusanya mapato wa Afya ,kazi ambayo bado inaendelea ,kusimamia mfumo wa mapato (LGRCIS) na mfumo wa kukusanya mapato wa Hospitali ,kuingiza kata zote za Halmashauri ya Mji, shule za msingi na majina ya walimu wakuu kwenye mfumo wa usimamizi wa elimu ya Msingi(PREM) kwa ajili ya usajili wa wanafunzi wa shule za msingi,kusimamia mafunzo ya mfumo wa takwimu za walimu na wanafunzi kwa shule za msingi ,kuendesha mafunzo ya mfumo wa mapato na kuwasajili kwenye mfumo wa kukusanya mapato wakusanyaji ushuru katika kata za Muhunga ,Kumsenga na Murubona.

- Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Halmashauri ya Mji wa Kasulu imepanga kukusanya na kutumia jumla ya Tshs. **8,625,012,200.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Fedha hizo zinategemewa kutolewa na Serikali Kuu, Wafadhili na Mapato ya Ndani ya Halmashauri. Kulingana na bajeti ya mwaka 2016/2017, katika Kipindi cha Julai – Machi, 2017, jumla ya Tshs **2,832,343,066.28** zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 32.8. Hivyo utekelezaji wa bajeti ya miradi kwa mwaka 2016/2017 ni 30%. Fedha hizo zimepokelewa kutoka katika vyanzo vya Ruzuku ya Maendeleo (LGCDG), Mfuko wa Jimbo (CDCF), Mapato ya Ndani (OWN SOURCE), Fedha za Jengo la Utawala, Mfuko wa Pamoja wa Afya (HSBF), UNICEF, TASAF, EQUIP na Mradi wa THPS . Fedha nyingine zilizopokelewa katika kipindi hicho ni Tshs. **1,451,421,414.72** kutoka vyanzo vya Mfuko wa Barabara (miradi ya 2015/2016),fedha za THPS, P4R na Serikali Kuu. Fedha za miradi zilizopokelewa shuleni Halmashauri kupitia shule zake katika kipindi cha robo ya kwanza na ya pili ilipokea jumla ya Tshs. 526,000,000.00 kwa ajili ya shule za msingi za Mwenge, Juhudi na Buha na shule ya sekondari ya Buha. Katika kipindi cha robo ya Tatu, shule ya sekondari ya Bogwe imepokea jumla ya Tshs 318,000,000.00 na hivyo kufanya jumla ya Tshs. **844,000,000**. Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa katika kipindi cha Julai-Machi, 2017 ni kama

ilivyooneshwa hapo chini. Miradi iliyotekelezwa ipo katika **kiambata A** miradi unayosubiri fedha kwa ajili ya utekelezaji ipo katika **kiamabata B**

- Kitengo cha manunuzi kimefanya manunuzi ya mikataba mikubwa yenye jumla TZS **1,235,452,500/-** midogo yenye jumla ya **TZS 194,176,204/-** na kati ya hizo kiasi cha **TZS 82,688,788/-** kilikuwa kimelipwa na kiasi cha **TZS 26,834,416/-** bado kinadaiwa na wazabuni mbalimbali na Kusimamia taratibu zote za manunuzi yaliyofanyika katika idara zote za Halmashauri ya Mji. Ikiwa ni pamoja na Kutoa tangazo la zabuni kwa miradi ya barabara.
- Kamati ipitisha ombi la kutumia kiasi cha Tshs.**9,000,000/=**kwaajili ya vifaa vya kufungia mfumo wa mapato ya hospitali ya Mji kasulu. Mkuu wa Idara ya Afya Kinga na Tiba aliwasilisha ombi la kutumia kiasi tajwa hapo juu kwaajili ya kununulia vifaa vya kufungia mfumo wa mapato (GoT-HoMIS) hospitali ya Mji wa Kasulu ikiwemo kompyuta,Printer I na UPS,ambapo shughuli hii haikuwekwa katika bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2016/17.
- Kamati ilijadili na kupitisha kiasi cha Tshs. Tshs.**1,000,000,000.00** fedha iliyoletwa kwa lengo la Ujenzi wa Grand High School.aidha katibu aliwaslisha majengo yatakayojengwa ikiwa ni pamoja na Jengo la Utawala ,ujenzi wa Vyumba Vinne (4) vya madarasa na samani zake, Vyumba (3) vya maabara na samani zake ,Vyoo matundu nane (8) vya wananfunzi katika eneo la kufundishia, Mabweni mawili moja la wasichana na jingine la wavulana yenye vitanda 48 kila moja na vyoo, Bwalo la chakula,Jiko na stoo ya vyakula pamoja na samani zake, Nyumba nne (4) 2 in 1 za walimu nane na Nyumba moja ya Mkuu wa Shule. Hata hivyo ujenzi huu umekwishaanza na ujenzi unatekelezwa na JKT kambi ya Mtabila na kusimamiwa na Mhandisi wa Halmashauri ya Mji-Kasulu kwa njia ya kikosi kazi (force Akaunti).
- Kuhusu suala la vibanda vya stendi ya Murusi:-Mkurugenzi aliwajulisha wajumbe kuwa wafanyabiashara pamoja na wamiliki wa vibanda vilivyopo stendi mpya, wameanza kulipa kodi ya pango na mwitikio kwa wafanyabiashara hao ni mzuri wameendelea kujitokeza na kulipa kodi ya pango ambayo kwa mwezi wanatakiwa kulipa kiasi cha **Tshs.10,000**/= .

- Kamati ilipitisha Mabadiliko ya mtia saini kwenye akuanti za Halmashauri ya Mji-Kasulu kutoka Bw. Sungwa S.Mkenya (aliyekuwa kaimu Mweka Hazina wa Halmashauri ya Mji-Kasulu) na kuwa Bw. **Kasimu M.Ismail** ambaye kwa sasa ndiye mweka Hazina wa Halmashauri ya Mji wa Kasulu.Hali hii ilisababishwa na uhamisho kwa baadhi ya watumishi kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine.
- Kamati ilipitisha pendekezo la kutumia mawakala kukusanya ushuru wa mabango,maegesho ya magari na minala ya simu pamoja na madini ya ujenzi.Hii

ni kutokana na ufinyu wa watumishi katika ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri,uhaba wa vitendea kazi (magari) pamoja na gharama kubwa ya ufuatiliaji.

- Katika kipindi cha robo ya tatu, Idara ya Utawala na Utumishi imeendelea kusimamia shughuli mbalimbali zikiwemo za kiutawala na kiutumishi kwa ujumla katika ngazi ya ofisi na hadi ngazi ya kata na mitaa.Hata hivyo imeendelea kusimamia maadili na nidhamu ya watumishi mahali pa kazi,masilahi mbalimbali kama likizo,Uhamisho na stahili zingine za watumishi zilizopo kwa mujibu wa sheria,kanuni na tararibu za utumishi wa Umma.Halmashauri hadi kufikia tarehe ya kikao hiki inahitaji watumishi **2276**,waliopo ni **1703** na mapungufu ni watumishi **573.** Aidha Halmashauri katika bajeti ya mwaka 2016/2017 ilitenga nafasi wazi 652 kwa ajili ya kutatua changamoto ya upungufu wa Watumish**i**. Watumishi waliohamia ni kassim Mkama Ismail (Mweka Hazina) kutoka Halmashauri ya Tunduru na Nolasco Remijo Masava (Kaimu Afisa Mipango Miji) kutoka H/W Mkinga.Waliohama ni Juliana Letara (Afisa Mipango Miji) kwenda H/W Longido na Bw.Sugwa Mkenya (aliyekuwa kaimu Mweka Hazina) kwenda H/W Shinyanga. Pia kumefanyika uhamisho wa ndani kwa watumishi 45 kati yao ni walimu wa shule ya msingi 42 na shule ya sekondari 3. .Jumla ya Watumishi 7 wamestaafu ikiwa jumla ya watumishi **7** kutoka Idara ya Elimu Msingi . Kamati imepitia na kuridhia mkataba wa huduma kwa wateja pamoja na sera ya TEHAMA.
- Shughuli zilizofanywa na kitengo cha Sheria ilikuwa ni kuendesha mashauri mbalimbali katika Mahakama mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mahakama ya Wilaya ya Kasulu,Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Kigoma na Tume ya Usuluhishi Kigoma (C.M.A).pamoja na kutunga sheria ndogo,ikiwa sheria ndogo hizo ni kama zinavyoonekana hapa, Sheria ndogo ya Kodi ya majengo za halmashauri ya Mji wa Kasulu za mwaka 2016/2017, Sheria ndogo za Usafi wa mazingira za Halmashauri ya Mji wa Kasulu za mwaka 2016/2017,Sheria ndogo za (Ushuru wa Stendi) za Halmashauri ya Mji wa Kasulu za mwaka 2016/2017, Sheria ndogo za (Ushuru na kodi za madini ya ujenzi)) za Halmashauri ya Mji wa Kasulu za mwaka 2016/2017, Sheria ndogo ya (Uanzishwaji wa mfuko wa afya ya jamii) za Halmashauri ya Mji wa Kasulu za mwaka 2016/2017.Sheria ndogo hizi zipo kwenye kata kwa ajili ya kukusanya maoni ya wananchi.

Mhe.Mwenyekiti Naomba kuwasilisha.